Sauti Elimu

hakielimu

Toleo la 7
2004

ISSN 0856 8588

HakiElimu • Mtaa wa Mathuradas Na 739 • SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (255 22) 2151852 au 3 • Fax: (255 22) 2152449 • Barua Pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org

Watu wenye ulemavu wana uwezo

Na Rakesh Rajani, Mkurugenzi Mtendaji, HakiElimu

Ikiwa nitakwenda Ufaransa, ninaweza kupata wasiwasi mgumu. Mathalan, sitaweza kufahamu niparde basi gani. Nitahangaika pia kuagiza chakula kwenye mgahawa. Shuleni, sitaweza kufuatilia anachofundisha mwalimu wala kusoma vitabu. Nikikwama, sitaweza hata kuomba msaada.



Nitahangaika sana nikiwa Ufaransa si kwa sababu ya ujinga, au kuwa na matatizo au kwamba nina dosari. Nitasumbuka kwa vile siwezi kuongea Kifaransa hali niyo

inafanya mazingira kuwa magumu kuligana na mahitaji yangu.

Nikipanda mlima Kilimanjaro nikiwa nimevalia nawazi ninayotumia kila siku niwapo Dar es Salaam, nitapata matatizo. Nitashindwa kufika kileleni, si kwa sababu ya udhaifu, uvivu au kukosa uwezo. Nitashindwa kwa vile sina vifaa sahihi vya kupandia mlima Kilimanjaro. Ninahitaji nguo za baridi viatu maalum, chupa kubwa za maji na miwani ya jua.

Mifano hiyo miwili inadhihirisha kwamba mara nyingi watu hawana matatizo taklni mazingira yanawazuia kunyesha umahiri wao.

Mpe mlemavu asiyeona kitabu chenye maandishi maalum (Braille) na ataweza kukisoma. Jifunze lugha ya ishara na mlemavu asiyesikia ataweza kuwasiliana nawe. Jenga njia maalum za kupanda juu katika majengo ya ghorofa na mlemavu anayetumia baiskeli maalum ataweza kupita bila matatizo.

Watu wenye ulemavu wana uwezo. Tatizo ni mazingira yaliyojengwa na jamii ambayo inachukulia kwamba watu wote wana mahitaji sawa. inabagua watu wenye ulemavu. Tatizo lingine ni mtizamo wa jamii unaowadharau watu wenye ulemavu.

Watu wenye ulemavu hawahitaji kuonewa huruma. Wanahitaji heshima na nafasi ya kushiriki kikamilifu ndani ya jamii. Tunafanya nini kuhusu hayo?

Tuondoe vikwazo vya kielimu kwa wanafunzi wenye ulemavu

Na Palemon Rujwahula, CHAWATA, Dar es Salaam

Wakati tunajivunia mafanikio ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) kwa kiasi fulani, manitaji ya wanafunzi wenye ulemavu wa viungo bado hayajapewa uzito unaostahili.

Kwanza, shule nyingi zilizojengwa chini ya MMEM hazina vyoo maalum kwa ajili ya watoto wanaotembaa kutokana na ulemavu au wanaotumia magongo na viti vya magurudumu. Madarasa mengine yanejengwa sehemu za mlinuko na yana ngazi ndefu! Haya yote humfanya mtoto mwenye ulemavu kupaona shule kama sehemu ya mateso.

Pili, idadi ya wanafunzi wenye ulemavu wanaoandikishwa kuanza darasa la kwanza na hata sekondari bado ni ndogo. Si rahisi kupata takwimu zinazoonyesha idadi ya watoto wenye ulemavu; wangapi wanaziliwa kila mwaka? Wanaoandikishwa kuanza shule? Ni wangapi wansohitimu masomo? Nani anafualiia?

Tatizo hilo linaanzia kwenye utambuzi wa idadi ya watoto wenye ulemavu wa viungo waliopo katika vitongoji au vijiji. Watoto wengi wenye ulemavu huzaliwa kwenye familia maskini sana. Umaskini husababisha watoto hao kukosa elimu. Wazazi wao wanashindwa kuwapatia vifaa muhimu kama viti sare, viatu na hata nyenzo za kutembelea kama baiskeli maalum.

Jami pia bado ina mtazamo potofu juu ya watu wenye ulemavu; wanaendelea kuitwa majina ya kuwedhallisha! Baadhi ya walimu hawafahamu jinsi ya kufundisha watoto wenye ulemavu kulingana na aina ya ulemavu walionao. Idadi ya walimu wa watoto wenye ulemavu nchini ni ndogo. Nchi nzima kipo chuo kimoja tu cha Patandi, Arusha! Tutaondoaje vikwazo vya kielimu kwa wanafunzi wenye ulemavu?

Unahisi vipi ukiitwa majina ya kukudhalilisha?

Na Henry Wimile, Kituo cha Habari juu ya Ulemavu (ICD)

Makabila mbalimbali hapa nchini yamekuwa yakitwaita watu wenye ulemavu majina ambayo yanawadhalilisha na kufanya jamii kwaone kuwa hawana faida.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2000 na Dk. Ely Macha katika mikoa ya Dodoma na Tabora, walemavu wa viungo huitwa 'furu' yaani kobe. Jina la kobe linatokana na mwendo wanaotembea watu wenye ulemavu wa viungo. Mtu asiyeona huitwa 'kivimbi' yaani mti. Hi inamaanisha kwamba hawezi kusogea mahala alipo bila msaada.

Baadhi ya makabila huita watu wenye ulemavu wa akili maiti au zazeta na albino pia huitwa mzungu mwitu. Kwa ujumla, kila kabila lina namna yake ya kumtafairi mtu mwenye ulemavu. Majina hayo ya kudhalilisha yanaifanya jami isione umuhimu wa kuwasendeleza watu wenye ulemavu

Hapa nchini, ipo dhana potofu kwa baadhi ya makabila kwamba watoto wenye ulemavu husababisha mikosi katika familia. Ipo mifano halisi ambapo watoto wenye ulemavu wamekuwa wakiuawa. Wamasayansi pia, kwa kile wanachoita 'kufanya dunia iwe mahala bora', wanafanya utafiti utakaowawezesha kuharibu mimba zitakazoonyesha watoto watakaozaliwa kuwa na ulemavu.

Huu ni ukiukaji wa hak za binadamu. Je, watu wenye ulemavu hawastahili kuwepo duniani? Kwa nini binadamu atoe uhai wa mtu mwenye ulemavu? Je, wewe unamchukuliaje mtu mwenye ulemavu? Utajisikiaje ukiitwa majina ya kukudhalilisha?

Tuwajali wenye ulemavu

Na Eva Biswalo, SLP 70316, Dar es Salaam

Takwimu za leadi ya watu zinaonyesha kuwa asilimia 10 ya watu duniani ni wenye ulemavu. Kundi hilo linajumuisha aina zote za ulemavu. Katika aina zote hizo wanaoathirika zaidi ni wenye ulemavu wa akil.

Asilimia 90 ya watu wenye ulemavu wa akili hawawezi kuzungumzia hata wala mahitaji yao wenyewe. Wazazi, walezi na wanajamii huzungumza kwa niaba yao.

Hata hivyo, mtazamo potofu, imani za uchawi na ujinga wa baadhi ya watu katika jamii vimesababisha kutengwa kwa watu wenye ulemavu wa akili. Wazazi wengi, hata walio na elimu na uwezo kiuchumi, hawatoi huduma zinazostahili kwa watoto au ndugu zao wenye ulemavu huu.

Watu wenye ulemavu wa akili wamekuwa wakionekana kama mzigo katika familia zao. Baadhi ya wazazi na walezi hawaoiewi haki za watoto wao. Mia mwenye ulemavu wa akili anaweza pia kupatiwa elimu inayomsaida kujimudu kadri ya upeo wake.

Mfaala ilycpo hazingati watu wenye ulemavu wa akili: wengi hukaa katika shule za msingi kwa miaka kumi au zaidi wakijifunza kusoma, kuandika na hesabu bila ya kueiewa chochote. Huu ni uhibitisho kwamba wengi wao hawafaiyaweza masomo hayo hata wakikaa miaka 20!

Nashauri kuwa mtaala wa watu wenye ulemavu wa akili uachwe wazi au ulegezwe. Wenye ulemavu wa akili wana vipaji vingi. Hivyo basi, mtoto aangaliwe uwezo wake ndipo aendelezwe katika ujuzi au eneo anaiolitweza. Wakati umefika kwa jamii kuwajali watu wenye ulemavu wa akil

Jamii ijifunze kuishi na walemavu viziwi wasioona

Na Angelica P. Mtwale

Ulemavu wa kutoona, kutosikia na kutozungumza haufahamiki kwa watu wengi hapa nchini. Hebu fikiria jinsi ambavyc mtu mwenye ulemavu wa viungo kimoja anavyopata matatizo kuyakabili maisha. Lipo kundi la watu ambao ni viziwi wasiona na hawawezi kuzungumza.Watu wenye ulemavu wa aina hii wanapata matatizo makubwa!

Kutokana na kuwa na aina nyingi za ulemavu, jami hudhani kwamba watu viziwi wasiona hawawezi kueliimishwa. Lugha ya mawasiliano au mpapaso ni ngumu. Hata pale inapotokea kuwa wazazi wanataka mtoto mwenye ulemavu wa aina hii kupata elimu hujikuta hawana pa kumpeleka. Shule ya Uhuru Mchanganyiko ya jijini Dar es Salaam ndiyo pekee. Inayotoa elimu kwa watoto viziwi wasioona.

Mtoto akishapata elimu katika shule hiyo ya Uhuru na kuhitimu, hata akifaulu hujikuta hana pa kwenda. Hakuna vyuo wala shule za sekondari zenye walimu wanaoweza kufundisha watoto viziwi wasiona. Viziw wasiona pia hushindwa kuwasiliana na walimu, jami na hata wenzao kwa lugha ya mpapaso.

Nashauri vyuo vya Ualimu viwe na idengo cha viziw wasiona. Picha na habari kuhusu watoto viziw wasiona wakiwa darasani ziandikwe na kusambazwa kupitia vyombo vya habari. Hi itawezesha jamii kutambua kuwa watoto hao pia wana haki na wanastahili kupata elimu kama wengine. Jamii inayowazunguuka watoto viziw wasiiona ijifunze na kutilia mkazo lugha ya mpapaso!

Shiriki Shindano juu ya Ulemavu na Elimu

HakiElimu kwa kushirkiana na mashirika ya ICD, CHAVITA na SHIVYAWATA inazindua shindano juu ya ulemavu na Elimu. Lengo la shindano hili ni kuadili matatizo yanayowakabili watu wenye ulemavu katika elimu na kutoa mifano halisi ya jinsi matatizo yao yanavyoweza kushughulikiwa katika jamii zetu.

Shindano hili linalenga kuuliza maswali makuu mawili. Majibu ya maswali yazingatie hali halisi inayojitokeza katika eneo lako. Mawazo yako na uzoefu weko katika sehemu unayoishi vinahitajika kusaidia jamii kuboresha hali ya watu wenye ulemavu nchini.

Kila mmoja wetu, bila kujali umri, jinsia, kazi, dini au mahali anapotoka anakaribishwa kushiriki katika shindano hili. Kwa maelezo zaidi ya jinsi ya kushiriki, tafadhali tazama ukurasa wa pili wa jarida hili.



SautiElimu



Ulemavu na Elimu!

Shindano

Jibu maswali yafuatayo


1. **Eleza matatizo yanayowakabili watu wenye ulemavu katika elimu**
2. **Eleza mfano halisi wa jinsi ya kutatua matatizo hayo**

- Insha yako isiwe zaidi ya kurasa mbili (swali moja kwa kila ukurasa)
- Unaweza kupiga chapa au kuandika kwa mkono
- Unaruhusiwa pia kutumia michoro kama ukipenda
- Katika kila ukurasa andika jina lako, umri, jinsia na anuani kamili
- Tuma insha yako kwa *Ulemavu/HakiElimu Shindano* •SLP 79401• Dar es Salaam au kwa barua pepe: info@hakielimu.org



Zawadi

- Washindi 10 watapata zawadi ya Shilingi 200,000/- kila mmoja (shilingi 100,000/- atabaki nazo na 100,000/- zitakwenda kwa shule atakayoichagua)
- Kila mmoja wa washiriki 100 waliofanya vizuri atapatiwa machapisho
- Mawazo ya washiriki yatachambuliwa na kutengeneza kijitabu *(Michango na mawazo yote yatabaki kuwa mali ya waratibu wa shindano)*



Isaidie jamii yako kuboresha elimu kwa watu wenye ulemavu! Mawazo yako yanahitajika!